



UTHIBITISHAJI WA MADEREVA NI TIJA YA KUBORESHA USALAMA NA KUPUNGUZA AJALI ZA BARABARANI NCHINI


Na: Mambwana Jumbe

Ulishawahi kuijuliza ni madhara gani yanatokana na ajali za barabarani au taabu wanazopitia waathirika wa ajali? Na je, vipi kuhusu familia zinazobaki baada ya kupoteza wapendwa wao kama athari za ajali hizo?

Watu wengi hupitia wakati mgumu na kushindwa kuendelea na shughuli zao za kila siku kutokana na athari za moja kwa moja zinazotokana na ajali za barabarani mathalani kuwa majeruhi, kupata ulemavu wa maisha au hata kupoteza maisha. Athari hazipo tu kwa abiria wanaotumia vyombo hivyo vya usafiri pindi wanapopata ajali, bali kwa wamiliki wa vyombo pia hupata hasara kwa kuharibikiwa vyombo vya usafiri, Serikali hupata hasara kwa uharibifu wa miundombinu ya barabara na kuingia gharama za kufanya matengenezo. Mzigo huu hubewwa nasi sote kama Taifa tunapolazimika kutumia fedha za kigeni kununua magari mapya kama mbadala wa magari yaliyopata ajali, kununua vipuri na madawa kwa ajili ya kutibia majeruhi wa ajali hizo.

Kwa mujibu wa taarifa ya Jeshi la Polisi kuhusu TAKWIMU YA HALI YA UHALIFU NA MATUKIO YA USALAMA BARABARANI ya mwaka 2020, asilimia 91 ya ajali zinazotoka Tanzania Bara zinatokana na uzembe na makosa ya kibinadamu kama vile uendeshaji wa hatari, uzembe wa wa-

tumiaji wa barabara, mwendokasi na ulevi. Takwimu hizo zinaonesha vyanzo vingine vya ajali kuwa ni asilimia 5.7 inayochangiwa na ubovu wa vyombo vya moto na asilimia 2.7 inayochangiwa na sababu za kimazingira kama vile moto, vizuizi vya njia pamoja na ubovu wa barabara.



Takwimu ya Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani ikionesha hali ya vyanzo vya ajali za barabarani kwa mwaka 2020

Hali hii ilipiga kengele za hatari kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambapo mwaka 2019 Serikali iliipatia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) jukumu la kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa magari ya biashara. LATRA inatekeleza jukumu hilo kwa kuchukua hatua za ziada na kuanzisha mfumo wa kutahini madereva (Drivers Testing System - DTS) ili kuweza kupima maarifa ya madereva wenye leseni za kuendesha magari ya bi-

ashara. Hatua hii inalenga kusaidia kupunguza ajali za barabarani na kuhakikisha usalama kwa watumiaji wa huduma za usafiri wa barabara.

Akiuelezea mfumo wa DTS Kisheria, Mkuu wa Kitengo cha Sheria LATRA Bi. Selina Mloge anasema kuwa, Kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardini (LATRA) Sura ya 413 Kifungu cha (5) (1)(e), LATRA imepewa jukumu la kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wanaotoa huduma za usafiri kibiashara kama vile daladala, mabasi ya masafa marefu, malori, na kadhalika na pia LATRA ina wa-



Bi. Selina Mloge akielezea jukumu la LATRA Kisheria la kuwathibitisha Madereva na Kuwasajili wahudumu

jibu wa kuimarisha usalama katika Sekta zinazodhibitiwa ambazo ni sekta za usafiri wa barabara, usafiri wa reli na usafiri wa waya (cable transport).

Aidha, Bi. Mloge anaongeza kuwa, ili kufanikisha utaratibu wa kusajili na kuwathibitisha madereva na wahudumu, LATRA ilian-daa Kanuni zinazofahamika kama Kanuni za Kuthibitisha Madereva na Kusajili Wahudumu wa Vyombo vya Moto Vinavyofanya Kazi Kibiashara ambazo zilitangazwa katika Gazeti la Serikali Na. 81 la tarehe 7 Januari mwaka 2020.

Akizungumzia namna dereva anavyowezza kuthibitishwa, Bi Mloge anasema kuwa, kwa mujibu wa Kanuni za Kuthibitisha Madereva na Kusajili Wahudumu wa Vyombo vya Moto Vinavyofanya Kazi Kibiashara,

2020, kanuni ya (4)(1) inamtaka kila dereva anayeendesha chombo cha moto kibiashara awe amethibitishwa na LATRA, kufanya kinyume chake ni kosa kisheria.

Vilevile Bi. Mloge anasema kuwa, kwa mujibu wa Kanuni ya 22(2) dereva atakayeshindwa kukidhi masharti ya Kanuni hizo anatenda kosa. Endapo atahukumiwa atapaswa kulipa faini ya kuanzia elfu hamsini na isiyozidi shilingi laki mbili au kifungo kisichopungua miezi mita jela na kisichozidi mwaka mmoja jela au vyote faini na kifungo. Vilevile, alama zake (demerit points) zitapunguzwa kwa alama 10 kama ilivyoainishwa katika Jedwali la 5 Sehemu ya A kipengele cha 9 cha Kanuni za Kuthibitisha Madereva na Kusajili Wahudumu wa Vyombo vya Moto Vinavyofanya Kazi Kibiashara, (zilizofanyiwa Marekebisho) 2021.

Bi. Mloge anafafanua kuwa, pale ambapo dereva atabainika kuendesha chombo cha moto kibiashara bila kuthibitishwa na Mamlaka na kukiri kosa na kuomba kosa lake lififishwe adhabu yake itakuwa ni shilingi 50,000/=, vilevile atapunguziwa alama 10. Hii ni kwamba dereva akishathibitishwa atapewa alama 100 ambazo zitakuwa zinapungua akibainika na makosa mbalimbali na kwa kila kosa alama zitapungua kama inavyooneshwa kwenye Jedwari la 5 Sehemu ya A ya Kanuni za Kuthibitisha Madereva na Kusajili Wahudumu wa Vyombo vya Moto Vinavyofanya Kazi Kibiashara, (zilizofanyiwa Marekebisho) 2021. Hivyo, anawasihi madereva wajitokeze kwa wingi ili kuweza kuthibitishwa na kuepukana na kadhia zinazoweza kuwafika.

Naye Bi. Esnath Mwakyembe ambaye ni Kaimu Meneja Uthibitishaji wa Madereva na Usajili wa Wahudumu anaelezea mfumo wa DTS kuwa, ni mfumo wa kielektroni wa kutahini madereva, ambapo dereva anatakiwa kujisajili kwa kutumia namba yake ya NIDA kwenye mfumo mama wa RRIMS

kupitia anuani ya <https://rrims.latra.go.tz/> login na kuweka nafasi ya kufanya mtihani (booking) na kisha kuchagua tarehe na muda atakaopenda kufanya mtihani.

Vilevile anaongeza kuwa, ili dereva aweze kusajiliwa, anatakiwa kuwasilisha cheti cha chuo alichosomea udereva wa kuendesha magari ya biashara kutoka kwenye chuo kinachotambulika, nakala ya leseni yake ya udereva, uthibitisho wa kuliapia ada ya kuthibitishwa pamoja na taarifa ya daktari inayothibitisha afya yake na

kuchapisha cheti ambacho kitamtambulisha kuwa amethibitishwa na Mamlaka,” anafafanua Bi. Mwakyembe.

Aidha Bi. Mwakyembe anasema kwamba. “Tafiti mbalimbali zinaonesha kuwa chanzo kikubwa cha ajali ni makosa ya kibinadamu na hivyo Serikali kupitia LATRA infanya kila jitihada ili kupunguza ajali nchini hasa kwa vyombo vya abiria vinavyodhibitiwa na Mamlaka, kwani Mamlaka ina wajibu wa kuimarisha usalama katika sekta zinazodhibitiwa. Hivyo, inatumia teknolojia



Baadhi ya madereva waliojitekeza kufanya mtihani wa kuthibitishwa kielektroni inayofanyika katika vyumba maalum vya mtihani Makao Makuu ya LATRA, Dar es Salaam

taarifa hizi zote ataziwasilisha kwa njia ya mtandao kupitia mfumo wa RRIMS.

“Dereva atafika kufanya mtihani kwa kutumia mfumo wa DTS, mfumo utasahihisha mtihani na kutuma matokeo ya mtihani kwa dereva kwa njia ya ujumbe mfupi wa maadishi kupitia simu yake ya mkononi. Matokeo ya mtihani wa dereva aliyefaulu yatatumwa pia kwenye mfumo mama kwa ajili ya

za mifumo kama vile Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa Magari -VTS na DTS ili kutimiza wajibu huo.”

Vilevile, kuhusu mfumo unavyofanya kazi, Bi Esnath anawakumbusha madereva wote kuwa, mfumo hauruhusu udanganyifu wa aina yoyote kwa kuwa unasahihisha mtihani na kutoa matokea. Hivyo anawasihi madereva wote kufanya maandalizi ya ku-

tosha kwa kupitia mambo yote waliyosoma ili waweze kufanya vizuri katika mitihani, kwani mitihani hiyo imetungwa kwa kufuata mitaala ya vyuo vilivyopata ithibati ya kutoa mafunzo ya udereva”.

Naye Bw. Jerive Malaki, Afisa Leseni na Udhibiti LATRA anasema kwamba udereva ni fani ya kitaaluma kama zilivyo taaluma nyiningine ambazo vigezo na masharti ya kitaaluma huzingatiwa. Hivyo madereva walopitia mafunzo na kufuzu wanahimizwa kujitokeza ili waweze kuthibitishwa katika fani

Aidha, anasema kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu uwepo wa madereva wasiozingatia maadili ya fani ya udereva kwa kufanya kazi kwa mazoea hivyo kuchafua kazi na taaluma ya udereva. Mfumo wa kutahini madereva umekuja kutatta changamoto ya makosa ya kibinadamu yanayosababishwa na madereva wachache wasiozingatia taaluma ya udereva.

“Kwa kutumia Kanuni za LATRA za uthibitishaji madereva, thamani ya madereva itapanda na kuwafanya wafanye



Afisa usajili msaidizi Bi. Jackline Mwaipopo ambaye pia ni msimamizi wa mitihani (kushoto) akimuelekeza jambo mmoja wa madereva waliofika kufanya mitihani kwa ajili ya kuthibitishwa.


yao ya udereva. Zoezi la kuthibitisha madereva litasaidia kuwachuja na kubaki na madereva wenyewe uwezo na sifa stahiki za kuendesha magari ya kibiashara ili kuongezza tija na ufanisi katika sekta ya usafiri kwa njia ya barabara.

Bw. Malaki anaongeza kuwa, Serikali imefanya uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu ya barabara ambapo mikoa karibu yote nchini imeunganishwa kwa barabara za lami, hivyo ni muhimu kuwa na madereva wanaokidhi mabadiliko ya teknolojia na maendeleo makubwa tuliyonayo.

kazi kwa kujiamini, kwani hakuna dereva atakaye endesha gari la kibiashara kama hajathibitishwa na Mamlaka, hivyo upatikanaji wa dereva utapaswa kuzingatia utaratibu maalum hali itakayoondoa vitisho na kufukuzana bila utaratibu kwa madereva wanaozingatia maadili ya taaluma yao, Hivyo, madereva wasio na sifa hawatakuwa na nafasi tena,” anasisitiza Bw. Malaki.

Akizungumzia faida za mfumo huo, Mkurugenzi Mkuu LATRA CPA Habibu Sulio anaeleza kwamba, pindi dereva anayeedesha chombo cha usafiri kibiashara anaposajiliwa na kuthibitishwa na Maml-

ka atatambulika kwenye Jumuiya za Afrika Mashariki, COMESA na SADC. "Mataifa wanachama wa Jumuiya hizo yatakuwa na mfumo mmoja wa mafunzo, utahini na uthibitishaji madereva ambapo watakaokidhi vigezo watapewa vibali vinavyowaruhusu kuendesha gari katika nchi hizo endapo watakidhi vigezo vya kuingia nchi husika au kuajiriwa huko. Madereva waliothibitishwa na LATRA watanufaika na mfumo huu kwani vigezo vyao vimezingatia protokali za



Mwonekano wa mfumo wa RRIMS unaotumika kusajili madereva kwa ajili ya kufanya mtihani wa kuthibitishwa

Kimataifa."

Vilevile CPA Suluo anaongeza kuwa, dereva anayethibitishwa na Mamlaka atapatiwa kifaa maalum atakachotakiwa kukigusisha kwenye Mfumo wa Kufuatilia Mwenendo wa magari (VTS) kila anapoanza safari ambacho kitamsaidia kumkumbusha muda anaotakiwa kupumzika au kupokelewa kwakuwa anakuwa ameshaendesha kwa umbali ambao kitaalamu anakuwa amecho-ka.

Vilevile CPA Suluo anasema, uthibitishaji wa madereva utasaidia kuipandisha hadhi taaluma ya udereva ambapo ni vigumu kwa dereva mwenye uzoefu wa miaka 10 bila ajali kulingana na yule wa miaka 5 mwenye ajali kila mwaka mathalani. Hivyo zoezi hilo linatarajiwa kuwachuja madereva kul-

ingana na uzoefu na weledi kazini, hatua ambayo itasaidia sana kupandisha hadhi ya kazi ya udereva, tofauti na ilivyo sasa ambapo kumekuwa na malalamiko ya wamiliki kuajiri madereva wasio na sifa stahiki na hivyo kuchangia ajali za barabarani na kuishusha thamani ya udereva.

Naye Bw. Remmy Mbonda, dereva wa lori anasema kuwa kuna umuhimu wa kusajiliwa, kutahiniwa na kuthibitishwa na LATRA, anasisitiza, "Mtihani huu unamsaidia dereva kujitambua, fani ya udereva kutambulika rasmi na Serikali kumtambua dereva hivyo mimi kama dereva nitakua najiamini kwani natambulika rasmi, hivyo naweza kufanya kazi nchi yoyote. Niwasihii tuu madereva wengine wajitokeze kwa wingi na kuthibitishwa na LATRA."

Kwa mujibu wa CPA Suluo, mpaka sasa zaidi ya madereva 200 wamefanya mtihani na kati yao madereva waliokidhi vigezo vya kuthibitishwa na Mamlaka watapewa yeti vitakavyoambatana na masharti ambayo dereva hatatakiwa kuyavunja. Aidha, Kwa wale ambao hawakukidhi vigezo vya kuthibitishwa, wanapewa nafasi ya kuijandaa vizuri na kurudia mtihani ili kuhakikisha kila dereva anapata haki yake Kisheria ya kuthibitishwa na hivyo Serikali kupata matokeo chanya kwa kupunguza ajali zinazoweza kuepukika.

DEREVA WA CHOMBO CHA USAFIRI KIBIASHARA

FANYA

MTIHANI

UTHIBITISHWE

- Utambulike rasmi
- Ufungue fursa kimataifa
- Uimariske usalamu barabarani

JISAJILI KUPITIA
rrims.latra.go.tz

www.latra.go.tz ☎ 0800110019